## EPISODE 9 "BUSINESS GROWTH"

| | |
|---|---|
| **SCRIPT WRITER** | **Njoki Muhoho** |
| **EDITOR** | **Jan-Philipp Scholz** |
| **KISUAHELI:** | **Eric Ponda** |

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu's restaurant. |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George's uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **MUMBI** | 22 years old, Zapcom's cousin and social worker. Female. |
| **AUNTIE BONGI** | 45 years old, the local government Telecommunications company manager. Everyone calls him The Manager. |
| **CUSTOMER** | Young man. |

**INTRO**

1. **MUSIC: THEME MUSIC**

2. **ANNOUNCER** HUJAMBO MSIKILIZAJI WA DEUTSCHE WELLE MAHALI POPOTE ULIPO NA KARIBU

KWA MAKALA NYINGINE YA MFULULIZO WA VIPINDI VYA ‘LEARNING BY EAR’ TUKIWA BADO TUNAZUNGUMZIA TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA KIPINDI HIKI CHA TISA KWA JINA “USTAWI WA BISHARA.”

KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA, VIJANA WANAFUNGUA TOVUTI NA KURASA ZENYE PICHA CHAFU KATIKA MTANDAO, JAMBO LINALO MUUDHI MJOMBA KILU. AIDHA ANAWAFUKUZA PAMOJA NA BIASHARA YAO KUTOKA MKAHAWA WAKE WA KULA TU FOODS, NA KISHA KUWARUHUSU TENA BAADA YA MTEJA WAKE MAARUFU NA AMBAYE PIA NI MENEJA WA KAMPUNI YA KITAIFA YA MAWASILIANO KUINGILIA KATI SUALA HILO.PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KUDUMISHA MAADILI MEMA KAZINI..

LAKINI SASA WANAKUMBWA NA CHANGAMOTO KATIKA MASUALA YA USTAWI NA KUBORESHA BIASHARA YAO.JE WATAFAULU. ENDELEA KUWA NASI HADI MWISHO WA KIPINDI UFAHAMU NI CHANGAMOTO ZIPI KIBIASHARA ZINAZOWAKUMBA VIJANA HAWA.

**SCENE 1: KULA TU FOODS – INTERNET CAFE**

**3. A-SFX: COMPUTER KEYBOARDS AND MUMURING OF A BUSY INTERNET CAFÉ.**

| | | |
|---|---|---|
| **4.** | **ANNOUNCER** | Wateja wamesongamana katika kibanda cha huduma za intaneti kwenye mkahawa wa KULA TU FOODS. Komputa zote sasa zinatumika huku wateja wengine wakipiga foleni kusubiri huduma hizo. ZAPCOM na GEORGE wanaonekana wachovu baada ya kufanya kazi kwa saa nyingi kuliko ilivyo kawaida. |
| **5.** | **ZAPCOM** | **(EXHAUSTED)** George, hatuwezi kuendelea kufanya kazi hivi? Tumekuwa tukifanya kazi saa nyingi zaidi kila siku ya wiki. |
| **6.** | **GEORGE** | Zap, Najua umechoka! Mjomba Kilu sasa anafikiri nimeacha kazi yangu ya kuwahudumia wateja mkahawani. Sasa nitamudu vipi kazi zote hizi, mkahawa wa chakula hapa Kula Tu Foods, na kibanda cha huduma za Intaneti? Siwezi kuwa kila mahali wakati mmoja . Unaelewa? |

7. **UNCLE KILU** **(SHOUTING FROM FAR)** George, Unafikiri wateja watakusubiri wewe hadi saa ngapi?

8. **GEORGE** **(FRUSTRATED)** Nakuja mjomba.

9. **CUSTOMER** Wewee, Zapcom …! lakini leo tutahudumiwa kweli? Tumesubiri kwa zaidi ya dakika 25 sasa? Nafikiri bora uweke kipimo cha muda wa mteja kutumia kumputa…

10. **GEORGE** **(LOUD WHISPER)** … Zapcom Siwezi tena …. (**EXCITED**). Ohh..Mumbi ni wewe? Tumefurahi kukuona tena hapa..! tunakuhitaji sana…!

11. **MUMBI** Habari Zap, habari George…? Kwanini munaonekana wachovu hivi?

12. **ZAPCOM/GEORGE** Kwa sababu tume….!

13. **CUSTOMER** Wewe … njoo hapa unisaidie! Tunataka Komputa?

14. **UNCLE KILU** George kwani lazima nije nikuvute kwa kamba?

| | | |
|---|---|---|
| **15.** | **ZAPCOM** | **(RESIGNED)** Karibu sana Mumbi, karibu katika mkahawa huu wa Kula Tu Foods ambao sasa huduma zake zimeboreshwa. |
| **16.** | **GEROGE** | **(RUSHING**) Nyinyi wawili endeleeni kushughulikia tatizo hili, na mimi naenda kuwahudumia wateja! |
| **17.** | **MUMBI** | Zap, nafikiri sasa umefika wakati wa kupanua biashara yetu. |
| **18.** | **ZAPCOM** | Kupanua biashara? Ikiwa tayari sasa tunashindwa kutosheleza mahitaji ya wateja tulio nao, itakuwaje tuzungumzie suala la kupanua biashara hii? |
| **19.** | **MUMBI** | Inategemea mtazamo wako katika suala hili. Mimi nafikiria tu jinsi tutakavyoweza kuboresha zaidi huduma hizi mpya ili kupunguza msongamano katika kibanda hiki… |
| **20.** | **UNCLE KILU** | **(ANGRY AND YELLING)** George, wewe si mtu mkubwa kiasi cha mimi kutoweza kukuvuta masikio …! Hebu nenda upesi ukawahudumie wale wateja pale, wamezubaa kama ndizi sokoni!! |

| | | |
|---|---|---|
| **21.** | **MUMBI** | **(RESIGNING)** Ningependa kuwaalika mje ofisini mwangu kwa mazungumzo ya kutafuta njia bora za kuboresha huduma hizi za mtandao wa Intaneti. Najua nyote mumechoka na munahitaji muda wa kupumzika!. |

**SCENE TWO: MUMBI'S OFFICE**

| | | |
|---|---|---|
| **22.** | ANNOUNCER | Ama kwa hakika wote wanahitaji muda zaidi wa kupanga mikakati na mbinu za kuboresha zaidi biashara yao. Kutafuta huduma nyingine zaidi zinazopatikana katika teknolojia hii mpya ya mawasiliano, katika juhudi za kutatua shida zinazowakumba kwa hivi sasa. |
| **23.** | **MUMBI** | Asanteni sana kwa kufika kwenu. Nimewaomba wenzangu watupe muda kidogo japo wa kutosha tuweze kujadiliana na kutafuta njia bora za kushughulikia suala hili. |
| **24.** | **UNCLE KILU** | Binti yangu… hii ni ofisi kubwa na nzuri sana. Unajihisi vipi unapokuwa katika ofisi hii..?.hata hivyo hatutachukua muda mrefu!. |

| | | |
|---|---|---|
| **25.** | **MUMBI** | (**AUTHORITATIVELY**).Hebu pitieni kwa makini mapendekezo haya. (**PAPER SHUFFLING**). Tunapaswa kufungua matawi zaidi ili kuwawezesha wateja wetu kuwasiliana vyema na kwa urahisi zaidi na jamaa zao. Na ili kufikia hilo tunahitaji kufungua matawi katika vijiji vyote hapa wilayani. |
| **26.** | **ZAPCOM** | Mumbi, Mapendekezo haya umeyatoa mapema mno ….lakini endelea ..nasikiliza!. |
| **27.** | **MUMBI** | Napendekeza kuekeza zaidi katika mitambo ya Komputa, lakini tufungue matawi hayo mahali pamoja na wala sio kila lokesheni kote wilayani. Kisha tujaribu kuwafunza wateja wetu jinsi ya kutumia vyema vyumba vya mazungumzo mtandaoni. |
| **28.** | **UNCLE KILU** | Binti yangu Mumbi, sasa nimechanganyikiwa hata zaidi. Wakati mtakapoanza kuzungumzia suala la chakula , yaani kupika na kupakua ..na huduma nyinginezo mkahawani .. hapo nitaweza kuchangia!. |
| **29.** | **MUMBI** | Zap, mbona umenyamaza, kimya chako kina mshindo. |

**30. ZAPCOM** Nafikiria Mumbi, bado nalifikiria suala hilo… ni wazo zuri…! **(PAUSE)…** ***yahoo chat***, ***facebook, Hi5*** na tovuti nyingine yoyote ile iliyoko mtandaoni … nimeanza kuipenda zaidi huduma hii…

**31. UNCLE KILU** Nikupe chakula?

**32. GEORGE** **(IMPATIENT)** Hapana mjomba.. nitakula baadaye, … lakini unaweza ku………

**33. MUMBI** Zap, Nadhani unaelewa nina maana gani?.. na kila mahali tutakapoanzisha huduma hizi mjomba Kilu anaweza kufungua mkahawa mwengine wa Kula Tu Foods. Kwa kufanya hivyo biashara yetu itaimarika hata zaidi.

**34. ZAPCOM** Mumbi, tunahitajhi mapendekezo ya biashara.

**35. GEORGE** Kutoka kwa nani?

**36. MUMBI** Nitatafuta kielelezo cha mapendekezo kwenye Mtandao wa Intaneti. Nikipata nitajaza kisha tujadiliane.

**37. UNCLE** Msichana, yaonekana pia wewe umewahi kunywa supu ya mbuzi, sasa tunaweza kuendelea na kazi?

**38. ANNOUNCER** Wanatoka ofisini huku kila mmoja akitafakari yaliyojiri. Wanafahamu kwamba wana safari ndefu kujifunza mengi kuhusu Teknolojia hii mpya ya habari na mawasiliano na huduma zake, kabla ya kutimiza ndoto yao ya kubunisha matawi katika sehemu nyingine wilayani humo, ili kuwaunganisha watu wengi zaidi na hasa wanafunzi wanapokuwa likizoni. Na bila shaka hicho si kibarua rahisi.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE THREE: KULA TU FOODS INTERNET CAFÉ**

**39. ANNOUNCER** Sasa mapendekezo ya biashara yako tayari. ZAPCOM na Mumbi wamekuwa wakichunguza na kujadilia mapendekezo hayo, huku George akiendelea kuwahudumia wateja katika mkahawa wa chakula wa Kula Tu Foods.Omwa naye amekuwa akishughulikia wateja katika kibanda cha huduma za Intaneti.

**40. ZAPCOM** Nina wasiwasi kwamba wafanyi kazi wapya tutakaowaajiri hawatakuwa na ujuzi wa kutosha kuwahudumia na kuwapa mafunzo ya msingi wateja wetu kuhusu njia bora za kutumia huduma hizi.

**41. MUMBI** Hapo ni kweli kabisa, Zapcom. Tuna uhaba wa wafanyiakazi wenye ujuzi wa kutosha, na sisi hatuwezi kuwa kila mahali.

**42. ZAPCOM** (**LIGHT BULB MOMENT**) Najua mtu anayeweza kutusaidia. Hebu nimpigie simu!.

**43. B:SFX: PHONE KEY BOARD PUNCHING AND A LONG DELAY. ECHO OF A DISTANCE CALL.**

**44. ZAPCOM** Shangazi Bongi? Habari… …unanisikia… kuna kelele sana hapo ulipo…na… na….kwani uko wapi?

**45. AUNTIE BONGI** Habari za jioni Zapcom? Watu hawajambo nyumbani?

**46. ZAPCOM** Habari za asubuhi ni njema!…. lakini kwa nini unaniamkua habari za jioni?

**47. AUNTIE BONGI** Oh, ni jioni hapa. Mimi niko Marekani!.

**48. ZAPCOM** (**CONFUSED**)… Uko wapi..? Marekani ..? tangu lini?…Na inakuwaje… mimi nimepiga simu nikitumia nambari yako ya hapa nyumbani na bado nimekupata..! Kwani hutumii nambari za Marekani?.

**49. AUNTIE BONGI** Usiwe mjinga hivyo, simu yangu ya mkononi ni ile inayoweza kushika au kutumika kila mahali niendapo yaani ***roaming.***

**50. ZAPCOM** Nataka kukuuliza swali moja tu!. Hebu kwanza niweke kipaza sauti kwenye simu yangu. Mumbi na …. **( A GRUNT FROM GEORGE WHO HAS JUST ARRIVED**) George wako hapa na mimi!

**51. C: SFX-CRACKING AS HE PUTS ON THE SPEAKER. VOLUME INCREASES**

**52. MUMBI** Shangazi …tunahitaji msaada wako. Tunahitaji kuwafunza watu wengi zaidi ili watusaidie katika bishara hii yetu ya huduma za Intaneti hapa mkahawani na mingine tutakayoifungua kila mahali hivi karibuni.

**53. AUNTIE BONGI** Hakuna haja ya kuingia gharama hizo zote. Mnachohitaji kufanya ni kuwatafuta vijana wa chuo kikuu ambao wako likizoni. Wao hutumia Komputa chuoni na itakuwa rahisi kwao na kwenu pia. Na hakika watafurahia huduma hizo za Intaneti mbali na kujipatia riziki wanapokuwa likizoni……. munaweza tu kuwatafuta na kukubaliana.

**54. MUMBI** Wazo zuri sana shangazi Bongi.

**55. AUNTI BONGI** Samahani sasa muda wangu umekwisha, kuna watu wananisubiri. Lakini unaweza kuungana nami kwenye anuani yangu ya ***Facebook***. Nitakutumia habari na maelezo zaidi kuhusu mafunzo ambayo nimekuwa nikibadilishana na wenzangu katika matawi yetu yote kote ulimwenguni. Hivyo sio mimi peke yangu mtakayeweza kubadiishana habari bali na mtu yoyote mahali popote. Samahani lakini kwaheri kwa sasa.

**56. ZAPCOM** **(INTERRUPTS**) Shangazi .. tafadhali niletee….

**57. AUNTIE BONGI** **(AMUSED)** Kwaheri Zap….. Mumbi na George . **(CLICK)**

**58. MUMBI/ZAPCOM** WOW!

**59. GEORGE** *Facebook* ni nini?

F

**60. ZAPCOM** George, ***Facebook*** ni tovuti ya kijamii inayowaunganisha watu kutoka sehemu mbalimbali. Watumiaji wanaweza kubuni makundi ya kirafiki au wanafunzi katika eneo, mji au mahali popote pale na kubadilishana habari. Katika tovuti hii wanaweza kutoa maelezo yao kwa ufupi na kubadilishana mawazo, habari na matukio mbalimbali miongoni mwao.

**61. GEORGE** Kwani siri yangu nimueleze mtu mwengine?. Na kuna haja ya watu wengine kujua habari kunihusu?

**62. ZAPCOM** Swali zuri sana hilo! Mtu anapaswa kumfahamu vyema anayebadilishana naye habari, na pia habari zenyewe. Lazima ufikirie sana kuhusu namna ya kuhifadhi siri zako. Unaweza kuwaalika watu kujiunga na tovuti ya ***Facebook*** na pia wao kukualika katika mtandao yao. Ni uamuzi wako! Pia kuna tovuti nyingine za kijamiii kama vile ***Hi5…***

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE FOUR: KULA TU FOODS INTERNET CAFÉ**

**63. D-SFX: COMPUTER KEYBOARDS AND MUMURING OF A BUSY INTERNET CAFÉ.**

**64. ZAPCOM** **(RAPID TYPING)** Sasa chuo kinafungwa lini? Mwezi ujao…? (**TYPING**) Kwa nini unauliza?

**65. ZAPCOM** **(RAPID TYPING)** Kwa sababu nataka kukupatia kibarua. **(PAUSE)** Kufanya nini?

**66. UNCLE KILU** **(LOUD WHISPHER)** Sasa Zapu anafanya nini? Anaandika kwa Komputa, asimame na kuendelea tena huku akichapa kwa hasira herufi kwenye kibao cha komputa…..Natumai shinikizo hili halijamfanya ashikwe na wazimu….

**67. UNCLE KILU** Zapu, Kwani unazungumza na mashini?

**68. ZAPCOM** (**DISTRACTED AND TYPING AWAY**) Mjomba anawasiliana na Kamau. Unamkumbuka? Yule mto wa Jacob ambaye yuko chuo kiku jijini .

| | | |
|---|---|---|
| **69.** | **UNCLE KILU** | Hapana, Zapu, unaongea na Komputa, mbona simuoni Kamau?. |
| **70.** | **ZAPCOM** | Yuko hapa mjomba! |
| **71.** | **UNCLE KILU** | **(EXCLAIMS**) Asalalala! Mtoto umeshikwa na wazimu wewe! Zapu, simuoni Kamau hapa. yuko wapi?. |
| **72.** | **ZAPCOM** | **(STILL ENGROSSED)**... Hebu tazama, huoni mtu akinijibu. Tunawasiliana naye hivi sasa? |
| **73.** | **UNCLE KILU** | (**ASTONISHED)** Ni yeye? Anasemaje? Msalimie mwambie niko hapa. |
| **74.** | **ZAPCOM** | **(RAPID TYPING)** Kamau…. mjomba yuko hapa anakusalimu … unamkumbuka, mjombake George **(PAUSE)** |
| **75.** | **ZAPCOM** | Sasa unaona amenijibu. Hebu nikusomee ujumbe wake alioandika. "Habari mjomba Kilu, bado unapika ile supu tamu ya mbuzi?" |
| **76.** | **UNCLE KILU** | **(OVERWHELMED)** Yaani unazungumza naye sasa…! kwa kutumia vidole vyako tu… Ha ha! Zapu, muulize atakuja lini.. kunywa supu ya mbuzi..! fanya upesi… mwandikie umuulize!. |

**77. ANNOUNCER** Kila siku Mjomba Kilu anajifujifunza mambo mapya. Tangu kuwasili kwa teknolojia hii, ameona na bado anaendelea kuona manufaa yake kila dakika. Huduma inayompa faraja kila mmoja anayetumia. Na hivyo kuleta matumaini ya kupanua biashara ya kundi hili la vijana. Je faraja hii itawafikisha wapi?

Kwa mengi zaidi ungana nasi kwa kipindi kijacho cha Learning By Ear, Noa Bongo Jenga maisha yako upate kujua yale yatakayotokea kwenye makala ya 10 na ya mwisho kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu Teknolojia mpya ya habari na mawasiliano. Ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa!